# KANUNI ZA UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA (TANZANIA COMMITTEE CLERK S UNION)

## TACCU

**@2023**

REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

## Jina la kanuni

Kanuni hizi zitaitwa kanuni za UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA (TANZANIA COMMITTEE CLERK S ASSOCIATION) TACCA

## Tarehe ya kuanza kutumika

**1.** Kanuni hizi zitaanza kutumika tangu Umoja kitakapokuwa kimepata usajili kutoka kwa ofisi ya Msajili wa Jumuiya wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

## Matumizi Ya Kanuni

**2.** Kanuni hizi zitatumiwa na wanachama wa **UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA (TANZANIA COMMITTEE CLRKS ASSOCIATION TACCA )**

## SEHEMU YA PILI

### *UANACHAMA.*

### Namna ya kujiunga

4. (i) Itakuwa ni wajibu wa mwanachama mwombaji Kuomba kujiunga na umoja huu bila kulazimishwa na kwa hiari yake.

(ii) Mwanachama mwombaji atatakiwa kujaza fomu maalumu ya kujiunga kama inavyoonyeshwa hapa katika Jedwali hili.

## FOMU YA KUOMBA UANACHAMA

**(Kanuni ya 4(ii))**
**Fomu Na 1**

### *Sehemu ya kwanza*

1. Jina la mwombaji …
2. Umri
3. Kazi yake …
4. Kituo chake cha kazi Jiji/Mkoa/wilaya/ halmashauri .
5. Mwajiri wake (Jiji/Mkoa/Halmashauri) .. …
6. Mahali anapoishi .
7. Sababu za kuomba uanachama …
8. Zingatia maelezo unayosoma

Umeelewa katiba na kanuni **NDIYO / HAPANA** ☐



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

Utayari wa kulipa **ADA** na **MICHANGO** kwa kuwa nimeelewa katiba na kanuni naahidi kutoa / kulipa **ADA** na **MICHANGO** ya umoja kwa uwezo wangu wote na sitaacha kulipa **ADA** kwakuwa ndiyo inayonipa uhai wakuwa mwanachama hai wa Umoja huu.

9. Jina
10. Sahihi
11. Tarehe

(iii) Mwanachama atakayeomba atawajibika kulipia kiingilio ambacho kitakuwa;-.

(a) Ada ya Kiingilio cha Uanachama Tshs 50,000/=,

(b) Ada ya uanachama ya kila Mwezi Tshs 10,000/=

(iv) Baada ya ombi la mwombaji kukubaliwa atapatiwa kitambulisho cha uanachama kitakacho mtambulisha kuwa yeye ni mwanachama.

(v) Kwa wale waombaji watakao kataliwa katibu wa Umoja atawaandikia barua ya maandishi kuwataarifu kuhusiana na kukataliwa kwao akieleza sababu za kukataliwa.

### 5. Masharti ya kujiunga

a. Katika kujiunga na Umoja kutakuwa na masharti ya kujiunga kama yalivyo elezwa kwenye katiba ya Umoja, pia, mwombaji atalazimika kulipa
   - (i) Ada ya kiingilio Tshs 50,000/=
   - (ii) Ada ya Uanaumoja ya Mwezi Tshs 10,000/=

b. Mwanaumoja mpya atatakiwa kuisoma katiba ya umoja na kuelewa kabla ya kujiunga

c. Wanaumoja wa Umoja watakaomba kujiunga watakuwa na fursa sawa bila kujali ni muda gani wamejiunga.

## SURA YA TATU

## *UCHAGUZI NA TARATIBU ZA UCHAGUZI*

### 6. NAMNA YA KUWAPATA WAGOMBEA

a) Kutakuwa na Kamati ya Uchaguzi kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Umoja

b) Wagombea wa nafasi za viongozi watapatikana kwa kuomba uongozi na kujaza fomu za kugombea uongozi.

c) Kamati ya uchaguzi itapitia majina ya wagombea waliomba uongozi kwa kuzingatia sifa za kuwapata viongozi

d) Kamati ya uchaguzi itapitia majina ya walioomba uongozi na kuwapitisha wale wenye sifa ya kugombea.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

7. (1). Muundo wa Kamati ya uchaguzi utakuwa kama ulivyoelezwa katika Katiba ya Umoja.

(2). Kamati ya uchaguzi itakuwa na jukumu la kusimamia uchaguzi wa wagombea na kukamilisha uchaguzi mpaka kutangaza matokeo ya Uchaguzi.

## KAZI ZA KAMATI YA UCHAGUZI

**8.** (1) Kamati ya uchaguzi itakuwa na majukumu yafuatayo;

(a) Kusimamia Uchaguzi

**(b)** Kuhesabu kura.

(c) Kutangaza matokeo ya Uchaguzi.

### *Kutangaza matokeo ya uchaguzi*

9. (a) Matokeo ya uchaguzi wa viongozi yatatangazwa na Kamati ya uchaguzi baada ya kumaliza kuhesabu kura.

(b). Matokeo yatatangazwa pale pale Mkutano Mkuu utakapofanyika na uchaguzi utakapofanyika.

(c). Mwenye mamlaka ya kuwatangaza wagombea waliochaguliwa atakuwa mwenyekiti wa Kamati ya uchaguzi.

REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

# FOMU YA KUOMBA UONGOZI WA UMOJA

**(Kanuni ya 6 (b)**
**Fomu Na 2**
**Kanuni na**

## *Sehemu ya kwanza*

1. Jina la mwombaji
2. Umri
3. Mahali alipozaliwa
4. Kituo cha kazi Jiji/Mkoa/Wilaya/Halmashauri
5. Mwajiri wako Jiji/Mkoa/Wilaya/Halmashauri
6. Mahali anapoishi
7. Muda wake wa kuwa mwanachama

## *Sehemu ya pili*

9. Cheo / nafasi anayoomba
10. Sababu za kuomba
11. Elimu aliyonayo
12. Jina
13. Sahihi ya mwombaji ...............

## *Sehemu ya tatu*

Sehemu hii ijazwe na Mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi
Maoni ya Kamati ya uchaguzi

- ✓ Anasifa za uongozi
- ✓ Hana sifa za uongozi
- ✓ Apewe nafasi ya kugombea / asipewe hana sifa ya ungozi

14. Sababu za kukubaliwa / au kukataliwa

15. Jina la Mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi

Sahihi yake .Namba ya simu

Mhuri



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

(3) Wanachama waliogombea uongozi watajadiliwa na Halmashauri Kuu kabla ya kujinadi kuomba kura kwa wanachama wa Umoja kwenye Mkutano Mkuu wa Uchaguzi.

(4) Kamati ya kusimamia uchaguzi itawajibika kusimamia uchaguzi hadi utakapo kwisha.

(5) Mgombea aliyeshinda nafasi aliyoomba atapewa hati ya ushindi na kamati ya kusimamia uchaguzi.

## SURA YA NNE

### *USULUHISHI WA MIGOGORO*

**10.** (a) Kutakuwa na Kamati ya usuluhishi wa migogoro kama ilivyoelezwa katika Katiba ya umoja ambayo itakuwa nawajibu wa kusuluhisha Migogoro ndani ya Umoja.

(b) Majukumu ya kamati za maadili ni kama ifuatavyo;

i. Kusimamia maadili ya wanaumoja wote ndani ya Umoja.
ii. Kuhoji kuchunguza na kutoa maoni juu malalamiko yoyote yatakayowasilishwa juu ya Mwanaumoja yeyote aliyekiuka Maadili.
iii. Kusikiliza malalamiko kutoka kwa wanaumoja yanayohusu wanaumoja na mwanaumoja au mwanaumoja na uongozi wa umoja.
iv. Kutoa uamuzi juu ya mgogoro uliousikiliza
v. Kutoa nafasi ya kukata rufaa kwa mwanaumoja ambaye akuridhika na uamuzi wa Kamati.
vi. Kamati ya usuluhishi itaanda mwenendo wa mgogoro na kuwasilisha katika ngazi ya rufaa ambayo mwanaumoja amepeleka malalamiko yake.
vii. Mwanaumoja ambaye atakuwa ajaridhika na Adhabu aliyopewa na Umoja atakuwa na Haki ya kukata rufaa katika vyombo vingine vya kutoa haki vya nchi kama ilivyoainisha katika Katiba ya Umoja.

## SEHEMU YA TANO

### *MIKUTANO NA TARATIBU ZAKE*

#### Aina Za Mikutano

**11.** Chama hiki kitakuwa na aina tatu za Mikutano kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Umoja.

(a) Kamati Tendaji
(b) Mkutano Mkuu wa Umoja
(c) Mkutano wa dharula.

#### Namna Ya kufanya Mikutano

**12.** (1) Mikutano itafanywa kwa kujadili mambo muhimu ya kujenga umoja kwa

a) Kujadili utoaji wa Ada.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

b) Kujadili wanachama waliofanya makosa kuwachukulia hatua.
c) Kufanya uchaguzi wa viongozi kipindi cha uchaguzi.
d) Kujadili namna ya kufikia malengo ya Umoja kama yalivyoelezwa katika Katiba.
e) Kupitisha wanachama wapya baada ya Kukubaliwa.
f) Kuwafuta wanachama baada ya kuthibitika wametenda makosa

(2) Mahali na Muda wa kufanyika Mkutano husika itakuwa ni makubaliano yatakayofanywa na viongozi wakishirikana na wanaumoja.

### 13. Namna Ya Kufanya Mkutano Ya Dharura/maalum

a) Mkutano ya dharua itafanywa tu pale jambo la dharura lisiloweza kusubiri Mkutano Mkuu ama Mkutano wa Kawaida.
b) Pia, pale Mwenyekiti wa Umoja atakapoona inafaa kuitisha Mkutano huu.
c) Mkutano huu pia, utaendeshwa kama Mikutano mingine.

### 14. Mambo Yapasayo Kufanywa Na Wajumbe Wawapo Mikutanoni

a. Wajumbe wamikutano waliotajwa wanawajibu kujadili maswala muhimu kwa uwazi na upendo.
b. Ni marufuku kwa mjumbe yoyote kujadili swala lililoongelewa Mkutanoni nje ya Mkutano.
c. Jambo lolote lililojadiliwa ndani ya Mkutano litakuwa ni siri ya wajumbe, mjumbe yoyote atakaethibitika kutoa siri za Mkutano atachukuliwa hatua kali za kinidhamu.
d. Hatua zitakazochukuliwa dhidi ya majumbe Atakethibitika kutoa siri za mkutanoni.
   i. Kumundoa kuwa mjumbe
   ii. Kumvua madaraka ya uongozi aliyonayo
   iii. Kumpa karipio kali kwa barua.

**SEHEMU YA SITA**

## *ADHABU NA MAKOSA*

### Kutolipa Ada,

**15.** (1) Mwanaumoja atakayeshindwa kulipa ada ya kila mwezi atachukuliwa hatua zifuatazo

(a) Atalipa faini na Ada anayodaiwa kwa kadiri itakavyopitishwa na Mkutano Mkuu.

(b) Atafukuzwa uwanachama na kufutwa kwenye Daftari la chama kama atashinwa kulipa kwa kipindi kinachomnyima sifa za kuwa mwanaumoja.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

#### Kutofika Kwenye Vikao

**16.** (1) Mwanaumoja asipofika kwenye vikao bila taarifa atafanya kosa kubwa ambalo atachukuliwa hatua.

(2) Mwanaumoja asipofika kwenye kikao mfululizo anaweza kuondolewa katika Umoja na kufutwa kwenye daftari la umoja.

## SEHEMU YA SABA

### *UDHIBITI WA FEDHA ZA UMOJA*

#### Kuwepo Na Akaunti Ya Umoja

**17.** (1) Fedha zote za mfuko zituzwe banki itakayo kubaliana na wanachama kufungua akaunti.

(2) Malipo ya fedha yote yatafanyika kwa hundi ambazo zitasainiwa kundi A na kundi B ambao Watatokana na wajumbe wa kamati ya utendaji.

(3) Mtunza fedha atawajibika kuandaa taarifa za fedha kila mwaka na kutoa taarifa katika MkutanoMkuu.

#### Ukaguzi Wa Fedha

18. (1) Fedha za Umoja zitakaguliwa kwanza na Mkaguzi wa Ndani

(2) Mkaguzi wa nje wa fedha atachaguliwa na Mkutano Mkuu na kufanya kazi kwa maelekezo ya Kamati Tendaji.

(3) Mkaguzi wanje atawajibika kuandaa taarifa na za fedha na kuziwakilisha kujadiliwa na Mkutano Mkuu.

(4) Mkaguzi wa nje ni sharti awe mhasibu Anaetambulika na bodi ya wahasibu ya Taifa.

## SEHEMU YA NANE

### *MICHANGO NA TARATIBU ZA KUSAIDIANA KATIKA MASUALA YA KIJAMII*

#### UCHANGIAJI WA MFUKO WA UMOJA

a) Kutakuwa na Mfuko wa Umoja utakaochangiwa na wanaumoja wote;

b) Kila mwanachama atachangia kiasi cha shilingi laki moja na elfu ishirini (120,000). kwa mwaka.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

c) Uchangiaji utafanyika kwa awamu mbili yaani mwezi wa tano (Mei) na mwezi wa kumi na moja (Novemba) ya kila mwaka au pape ambapo umoja utaamua vinginevyo.

d) Mwanachama atatakiwa kuchangia kiasi cha shilingi laki moja (100,000) kabla au ifikapo tarehe 30, Mei ya kila mwaka na kumalizia kiasi kilichobaki cha shilingi elfu ishirini (20,000) kabla au ifikapo tarehe 30 Novemba ya kila mwaka pasipo kukosa.

## MAENEO YA KUSAIDIANA

(1) Mwanaumoja atachangiwa endapo atapatwa na mojawapo ya matukio yafuatayo:

a) Msiba
b) Harusi/Jubilei
c) Kustaafu

19. Mwanaumoja atachangaiwa kwenye tukio lililotajwa katika ibara ndogo ya 20 (1) endapo:

i. Tukio hilo litampata mwanaumoja mwenyewe, mtoto wa mwanaumoja, mwenza na/au mzazi.

ii. Kila mwanaumoja atatoa mchango wa rambirambi kwa kiwango kitakachopendekezwa na kuidhinishwa na wanaumoja katika Mkutano Mkuu.

iii. Mwanaumoja ambaye hatachangia misiba mitatu mfululizo endapo ikitokea amepatwa na msiba hatachangiwa na Umoja.

20. Tukio la harusi, mwanaumoja atachangiwa endapo:

i. Tukio hilo litamhusu mwanaumoja mwenyewe au mtoto wake wa kumzaa/Kumlea.

ii. Kila mwanaumoja atatoa mchango wa harusi kwa kiwango kitakachopendekezwa na kuidhinishwa na wanaumoja katika Mkutano Mkuu.

iii. Mtu mmoja hawezi kuchangiwa katika ndoa zaidi ya moja.

iv. Mwanaumoja ambaye hatatoa michango mitatu mfululizo endapo ikitokea ana tukio la harusi hatachangiwa na Umoja.

## *TARATIBU ZA KUSAIDIANA NA UTOAJI WA HUDUMA KWA WANACHAMA KUTOKA KATIKA MFUKO WA UMOJA*

24. Taratibu na viwango vya kusaidiana kutoka katika mfuko wa Umoja ni kama ilivyoainishwa katika Katiba hii na Kanuni za Umoja au kwa jinsi itakavyoidhinishwa katika Mkutano Mkuu.

25. Viwango vya kusaidiana ni kama vilivyoainishwa hapo chini au viwango vingine vitakavyoidhinishwa na wanaumoja katika Mkutano Mkuu. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo ;

a) Familia ya mwanachama aliyefariki kiasi cha Shilingi 200,000/= au pale umoja utakapo amua vinginevyo kupitia vikao vyake.

b) Mwanachama aliyefiwa na mtoto wa kumzaa na ambaye anatambuliwa kisheria kiasi cha Shilingi 200,000/= au pale umoja utakapo amua vinginevyo kupitia vikao vyake.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

c) Mwanachama aliyefiwa na mwenza wake wa ndoa anayetambulika kisheria na kwa taratibu za kiserikali kiasi cha shilingi 200,000/= au pale umoja utakapo amua vinginevyo kupitia vikao vyake.

d) Mwanachama aliyefiwa na mzazi wa kuzaliwa naye kiasi cha Shilingi 200,000/= au pale umoja utakapo amua vinginevyo kupitia vikao vyake.

e) Kwa mwanachama anayestaafu kwa mujibu wa sheria atapewa fedha kiasi cha Shilingi 300,000/= au pale umoja utakapo amua vinginevyo kupitia vikao vyake na au kulingana na sera ya fedha kwa wakati huo.

***NB:*** *Michango hii itatolewa tu kwa mwanaumoja aliye hai, yaani Yule ambaye amekuwa akichangia michango ya kila mwezi na ambaye amekuwa akiwajibiaka kwa kila shughuli ya umoja inayotangazwa. Hii ni pamoja na zile shughuli za kijamimi ambazo zitatolewa taarifa kwa wanachama wote kupitia viongozi wa umoja.*

## SEHEMU YA TISA

### *TARATIBU ZITAKAZOTUMIKA BAADA YA KUVUNJWA KWA UMOJA*

#### Ulipaji Wa Madeni

**27.** (1) Baada ya tamko kutolewa la kuvunjwa Kwa umoja , atachaguliwa mtafutaji madeni na mlipa madeni (debit collector) Atakaye chaguliwa na Mkutano Mkuu

(2) Katika kazi zake atakazofanya, atalipa madeni Kwanza ya Umoja.

(3) Katika kufanya kazi hiyo ya ulipaji madeni ambayo yanadaiwa na Umoja atawajibika kukusanywa madeni yote, fedha zilizobaki na mali zitagawiwa kwa Wanaumoja kama ilivyoelekezwa ndani ya Katiba ya umoja.

***HITIMISHO***

a) Kanuni hizi zinaweza kubadilika kutokana na matakwa ya umoja. Maamzi yatafikiwa na walau nusu ya wananchama au kuridhiwa na Mkutano Mkuu.

b) Mabadiliko yoyote ya kanununi hizi hayataathili malengo mahsusi ya umoja kama yalivyo ainishwa katika katiba ya umoja.

c) Kanuni hizi zitaanza kutumika pale tu umoja utakaposajiliwa na kutambuliwa rasmi kisheria kupitia mamlaka mbalimbali za kisheria.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS